ELIMU BATILI YA UWEZO
TATHMINI YA MAENDELEO YA MWANAFUNZI
MUHULA 1 001 – 2027
KISWAHILI INSHA
MUDA: DAKIKA 40

4

JINA: _____ **NAMBARI YA TATHMINI:** _____

SHULE: _____ **TAREHE:** _____

Umepewa dakika 40 kuandika insha yenye nakshi na ya kuvutia sana.

Andika insha kuhusu:

MWALIMU WANGU

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI – INSHA

GREDI 4 – MUHULA 1, 2027

Mada: MWALIMU WANGU

Jumla: Alama 20

A. MWONGOZO WA KUTOA ALAMA

Kipengele	Maelezo ya kuzingatia	Alama
1. Maudhui	Insha inahusu mwalimu; mwanafunzi amemtambulisha mwalimu na kueleza sifa, kazi au umuhimu wake	**6**
2. Mpangilio wa mawazo	Mawazo yamepangwa vizuri kuanzia mwanzo, kiini hadi mwisho	**4**
3. Matumizi ya lugha	Sarufi, msamiati, uundaji wa sentensi na matumizi sahihi ya maneno	**4**
4. Tahajia na uakifishaji	Tahajia sahihi, herufi kubwa, vituo, koma na alama nyingine za uandishi	**3**
5. Usafi na mwandiko	Mwandiko unaosomeka, kazi ni safi na imewasilishwa vizuri	**2**
6. Ubunifu	Matumizi ya lugha ya kuvutia, maelezo ya kibinafsi na mawazo ya mwanafunzi	**1**
JUMLA		**20**

Mwongozo wa jumla wa maudhui

Alama 6 za Maudhui:

- **6** – Ameeleza mada kikamilifu, maelezo ni mengi, yanahusiana na mada na yanaonyesha uelewa mzuri.
- **5** – Mada imeelezwa vizuri lakini kuna maelezo machache yaliyokosekana.
- **4** – Mada imeelezwa kwa kiwango cha wastani.
- **3** – Maelezo ni machache lakini mwanafunzi ameonyesha uelewa wa mada.
- **2** – Maudhui ni machache sana na hayajaendelezwa.

- **1** – Ameandika sentensi chache zinazohusiana kwa kiasi na mada.
- **0** – Hakujibu mada au kazi haiwezi kutathminiwa.

B. mfano INSHA YA ALAMA 20

MWALIMU WANGU

Mwalimu wangu anaitwa **Bi. Amina**. Yeye ni mwalimu wangu wa darasa. Ni mwanamke mwenye moyo wa upendo, subira na bidii. Kila siku huja shuleni mapema akiwa tayari kutufundisha. Yeye huvaa nguo safi na nadhifu na daima huwa na tabasamu usoni.

Mwalimu wangu hutufundisha masomo mbalimbali kwa njia rahisi na ya kuvutia. Anapotufundisha, hutumia mifano, picha na vifaa mbalimbali ili tufahamu vizuri. Ikiwa mwanafunzi hajamwelewa, humweleza tena kwa upole. Pia hutuhimiza kusoma kwa bidii na kufanya kazi zetu kwa wakati.

Bi. Amina anatufundisha kuwa na nidhamu, kuheshimiana na kusaidiana. Anapomwona mwanafunzi akiwa na tatizo, humsaidia kwa ushauri mzuri. Wakati wa michezo, hutuhimiza kushiriki na kufanya kazi pamoja. Kwa sababu hiyo, wanafunzi wengi wanampenda na kumheshimu.

Ninampenda sana mwalimu wangu kwa sababu amenisaidia kuwa mwanafunzi mwenye bidii na nidhamu. Ninapokua, ningependa kuwa mtu mwenye moyo wa kusaidia wengine kama yeye. **Mwalimu wangu ni mfano bora kwangu na nitathamini mafundisho yake daima.**

C. MFANO WA KUGAWA ALAMA KWA SAMPLE HIYO

Kipengele	**Alama alizopata**	**Maelezo**
Maudhui	**6/6**	Mada imeendelezwa vizuri na mwalimu ameelezewa kwa kina
Mpangilio wa mawazo	**4/4**	Utangulizi, kiini na hitimisho vimepangwa vizuri
Matumizi ya lugha	**4/4**	Sentensi zimeundwa vizuri na msamiati unafaa Gredi 4
Tahajia na uakifishaji	**3/3**	Tahajia na alama za uandishi zimetumika vizuri
Usafi na mwandiko	**2/2**	Ikiandikwa kwa mwandiko mzuri na usafi

Ubunifu	**1/1**	Maelezo yanaonyesha hisia na mtazamo wa mwanafunzi
JUMLA	**20/20**	**Insha bora**

D. VIWANGO VYA UTENDAJI

Alama	**Kiwango**	**Maelezo**
18–20	Bora sana	Mwanafunzi ameonyesha uwezo mkubwa wa kuandika insha
15–17	Vizuri sana	Mwanafunzi ameelewa mada na ameandika kwa kiwango kizuri
11–14 Wastani		Mwanafunzi ameonyesha uelewa lakini anahitaji kuboresha baadhi ya maeneo
		Maudhui na matumizi ya lugha yanahitaji msaada zaidi
1–6	Anahitaji msaada mkubwa	Mwanafunzi hajakuza mada ipasavyo na anahitaji mwongozo zaidi